

Zb-29-Nakutukuza ee Bwana

Kisha somo la Nne-Makesha ya Pasaka

Toni Iragi K

Solo/Tutti

Na - ku - tu - ku - za, ee Bwa - na, kwa ku - wa u - me - ni - o - ko - a.

4

1. Nakutukuza, ee Bwana, kwa kuwa umeniokoa,
wala hukuwafurahisha adui zangu juu yangu.

Ee Bwana, umeondoa roho yangu kuzimnuni,
umeniokoa katika wale wanaoshuka shimoni,

2. Mwimbieni Bwana, enyi waamini wake,
shukuruni jina lake litakatifu.

Kwani hasira yake ni ya kitambo kidogo,
mapendo yake yadumu maisha yote.

3. Usikie, ee Bwana, unihurumie,

ee Bwana, uwe msaada wangu.

Umegeuza kilio changu kuwa mchezo,

ee Bwana, Mungu wangu, nitakusifu milele.